2. Ukuta wa shule ya Nyota **u**li**o**jengwa mwaka uliopita **u**mepakwa rangi sasa. Ukuta huo **u**na michoro mbalimbali. **U**na michoro ya watu walio**zi**shika nyuta na mishale. Kuna pia **teo** **zi**li**zo**sukwa kwa njukuti **za** makuti na **zi**li**zo**sukwa kwa vijiti vya mikindu. Vilevile, kuna vyungu vya uji unaopakuliwa kwenye pawa. Pawa zenyewe ni **za** kumbi **za** nazi. Ni pawa **zi**na**zo**pendeza sana. Uga **wa** shule **u**mesimama katikati ya kuta nne **za** shule. Uga **u**na nyasi **za** kijani **zi**na**zo**pendeza. Kila unyasi **u**mesimama tisti kama mwanajeshi kwenye gwaride. Tosi **za** nyasi hizo **zi**mekatwa kwa ulaini wa ajabu! Kuna tepe **za** nyuzi **zi**li**zo**zungushwa kwenye kingo **za** uga huo mzuri.
3. ukuta, kuta, nyufa, ufa, ubavu, mbavu, uga, upinde, nyuga, pinde, unyasi, nyasi, uzi, nyuzi, utepe, tepe, utosi, tosi, ubao, nyanja, unyende, upeto, ushanga, ulimbo.
4. Kuta, nyuta, kwato, nyayo, kope, unyayo, ndimi, ukucha. Kingo, upawa, nyufa, teo.
5. *Kifungu kiwe kifupi chenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya U–ZI. Pia kihusu suala la misukosuko ya kijamii.*
6. Kwa mfano: Boriti lililokatwa jana lilipasuliwa mbao zilizonunuliwa zote pasi na kuwa na ubao hata mmoja uliosalia.
7. Kwa mfano: Uga na ukuta.

## X. Ngeli ya YA – YA

### Zoezi la 10

1. (a) **ya**li**yo**mwandama
(b) ali**yoya**onyesha

(c) **ya**li**yo**mpata
(d) **ya**taka**yo**tekelezwa
(e) **ya**li**yo**fanywa
(f) **ya**li**yo**andaliwa
(g) **ya**li**yo**mpata
(h) **ya**li**yo**mtatiza
(i) **ya**li**yo**waudhi
(j) **ya**li**yo**nukia

2. Marashi wakati mwingine **ya**nakuwa kero. Mtu aki**ya**nunua, ahakikishe kuwa **ya**naafiki mazingira ambapo ata**ya**tumia marashi hayo. Marashi **ya**naweza **ya**kawa usumbufu kwa watu hata kama **ya**tanukia. Maridhio **ya** watu **ya**naweza kukuonyesha kama marashi **ya**mependeza au la. Ikiwa manung'uniko **ya**takuwapo, basi ha**ya**po mapendezo **ya**na**yo**patikana katika marashi **hayo**. **Ya**siwepo mashindano **ya** watu kujipulizia marashi. Mashindano **ya** aina hiyo **ya**naweza kusababisha magonjwa na matokeo mengine hasi. Kwa kuwa wakati mwingine marashi **ya**naweza kuleta kichefuchefu na kisha matapishi, basi **ya**nastahili **ya**we **ya**kitumika kwa kiasi kidogo na kulingana na hadhira iliyopo.
3. mapumziko, maji, maradhi, matope, masizi, marejeo, mazingira, maridhio, maringo, masaibu, mashaka, mashindano, mashobo, mashtaka, masika, masikilizano, mazungumzo, maoni.
4. maji, maziwa, marashi, mafuta, makuu, maringo, matembezi, mazoea, mazishi, malumbano, Matilaba, maslahi, masimango, masengenyo, makombo, matamanio.
5. *Kifungu cha aya moja kizingatie upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya YA–YA. Kifungu hicho kihusu suala la misukosuko ya kijamii.*
6. matege, mateka, matembele, matembezi, matengenezo, matende, mateso, matibabu, matilaba, matlai, maktaba, maabara.
7. Kwa mfano: Maabara yaliyojengwa yalikuwa ya kisasa na yaliyovutia.

## XI. Ngeli ya LI

### Zoezi la 11

1.

(a) **li**na**lo**umiza
(b) **li**ingia**lo**
(c) **li**ua**lo**
(d) **li**tatiza**lo** hewa
(e) **li**sumbua**lo**
(f) **la** usingizi **li**hepa**lo**

2. Jua **li**kizidi sana joto huwa **li**napanda na watu wengi huumia. Lepe **la** usingizi **li**napotea wakati giza **la** usiku **li**naanza kushika kila mahali. Akili huanza ku**li**kumbuka vumbi **la** mchana **li**li**lo**kuwa **li**kivurugwa na upepo mkali.
3. jua, vumbi, giza, joto, vumba, jasho, jazo, lepe, jongo, jugwe, lamuka, vukuto.

4. Jua, joto, Vumbi, jasho, vumba, lepe, giza.
5. (a) *Zitungwe sentensi tano zinazozingatia upatanisho ufaao wa kisarufi wa nomino za ngeli ya LI. Kwa mfano:* Jua limewaka leo.
(b) *Sentensi zilizotungwa zisomwe ili zitolewe maoni.*
6. *Kifungu kiwe kifupi na chenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa nomino za ngeli ya LI. Kifungu hicho kihusu suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara.*

## XII. Ngeli ya KU

### Zoezi la 12

1.
   (a) Kulia ali**ko**lia
   (b) Kula ali**koku**la
   (c) Kufurahi ali**ko**furahi
   (d) Kutembea kwake kuzuri **ku**li**ko**wavutia watu
   (e) Kusubiri ali**ko**subiri
   (f) Kuhangaika **ku**kubwa **ku**li**ko**mpata
2. Kwetu **ku**li**ku**wa **ku**kinyesha mvua nyingi zamani lakini siku hizi **ku**mekauka kabisa. Mtu anaweza kudhani kuwa kwetu **ku**me**ku**wa jangwa kwa karne nyingi sana, kumbe si hivyo. Kulima **ku**me**ku**wa ghali kwa sababu ya **ku**kauka kwa ardhi. Kadhalika, siku hizi kwetu **ku**napandwa wimbi, mtama na mihogo kwa sababu ya kuadimika kwa mvua. Kutokana na **ku**kosekana kwa mvua au **ku**adimika kwa manyunyu ya mvua, **ku**me**ku**wa na **ku**hama kwa watu kutoka kwetu **ku**elekea mjini. Kuhama huko **ku**meongezeka sana kwa sababu hakuna anayekushutumu.
3. kuja, kuliwa, kuchoka, kupendeza, kutafuta, kuwa, kusahau, kudai, kuzuru, kunywa, kupwa.
4. Kufanya, kuwa, kubeba, kununua, kuuza, kuagizia, kusafiri, kulipia, kuagiza, kuweka, kutuma, kutoa, kuja.
5. *Kitungwe kifungu kifupi chenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa nomino za ngeli ya KU. Kifungu hicho kizingatie suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara.*
6. (a) Kwa mfano: Kutoroka kwake ndiko kulikomwokoa.
   (b) Sentensi zilizotungwa zisomwe darasani ili zitolewe maoni.

## XIII. Ngeli ya PA – KU – MU

### Zoezi la 13

1.
   (a) Mahali **hapo pa** watoto ni **pa**zuri.
   (b) Pahali **papa hapa** ndi**po** ni**pa**penda**po**.
   (c) Mahali **pale pale** ndi**po** nili**popa**taja.
   (d) Kuku **huku** ukweni ndi**ko** **ku**liko na starehe.
   (e) Mahali **kuko huko** mli**ko**toka ndi**ko** tuna**ko**enda.

(f) Mahali **humo** mna**mo**ingia ni **m**zuri.
(g) Mahali **m**na**mo**ingia ha**mu**fai.
(h) Mahali **mumu humu** ndi**mo** mahakamani.

2. Pahali **penye** watu wengi huwa **pana** uhai kuliko pahali **pa** watu wachache. Vivyo hivyo, ukienda **huko** Uzunguni **kwenye** baridi na uhaba wa joto la jua, utakuta **kuna** wenzetu **huko** ambao hawapendi mavazi mengi juu ya miili yao. Ukiingia nyumbani **mwao**, utakuta **humo** **muna** kila aina ya vyakula. Halikadhalika, **muna** vitu vya thamani. **Mule** ndani huwa **muna** makochi ya kila nui. Si kama Uswahilini **ambako** maisha huwa mepesi na ya kuchukulika.
3. huku, mahali hapa, huko, mahali huku, kule, mahali humu, humu, humo, mule, ujombani, ukweni, uzunguni, uswahilini, msituni, kambini, nyumbani.
4. Pahali, huku, mjini, ujombani, huko, pa akina Maliwaza, hapo, mahali, nyumbani, Shambani, humo, mwao akina Musa.
5. Zitungwe sentensi tano zinazozingatia upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya PA – KU – MU.
6. *Kitungwe kifungu kifupi chenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa nomino za ngeli ya PA– KU – MU. Kifungu hicho kizingatie suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara.*
7. (a) Kwa mfano: (i) Ameenda ujombani.

   (ii) Mahali hapa pana fujo.

   (iii) Ndani muna joto.

   (b) *Sentensi zisomewe wengine ili wazitolee maoni*.

## 3. Ukubwa na Udogo wa Nomino

### Zoezi la 1

1. jikombe, majilango, jidawati, jivulana, jikoba, majimeza, jidole, toto
2. (a) Majitoto, jitanda (b) Majipicha, jikuta (c) Jisufuria (d) majijumba, jishamba (e) majiatu, maguu
3. jisahani, majisu, jidarasa, jisichana, majitunda, majikochi, jichakula, jichwa, majitu, jiguo
4. (a) (i) jiwe – jijiwe (ii) redio – jiredio (iii) vitambaa – majitambaa (iv) kufuli – jikufuli (v) njia – jijia (vi) milima – majilima (vii) jukwaa – jijukwaa
(b) (i) jitabu (ii) jidawa (iii) jimoshi (iv) majishimo (v) jimchwa
5. (a) (i) Nimeliweka jisimu langu kwenye jifuko.
(ii) Majikalamu haya yanaandika vizuri.
(iii) Njoga alitumia jikaratasi lile kuandika jibarua/majibarua.
(iv) Jitambaa hili litatandikwa juu ya jikeka.
(v) Gombe/jigombe/magombe/majigombe na buzi/jibuzi/mabuzi/majibuzi yaliuzwa kwa jisoko.
(b) Tunga sentensi kwa kutumia nomino zifuatazo.
(i) goma/jigoma/magoma/majigoma (ii) jisherehe/majisherehe (iii) jikanisa/majikanisa (iv) domo/jidomo (v) dege/jidege/madege/majidege

### Zoezi la 2

1. kijikombe, kijijiko, vijilango, kijidawati, kijigari, vijimeza, kijidole
2. (i) Vijipaka, vijinyasi (ii) Kijiji, vijisherehe (iii) Kijivulana, vijibwa (iv) Kijichwa, vijinywele (v) kijibaiskeli, kijiduka
3. (a) (i) kijisaa/vijisaa (ii) kiguo/kijiguo/viguo/vijiguo (iii) kijidirisha/vijidirisha (iv) kijiji (v) kijijicho
(b) (i) Kijia/kijijia, vijishule (ii) kijibao, kijidarasa (iii) Kijirinda, vijidoa (iv) Kijito (v) Vibuzi/vijibuzi, vijibanda
4. (a) Kijisimu kilipotelea kwa eneo la kijisitu.
(b) Kijisiki kiliumiza kiguu/kijiguu chake.
(c) Kijikuta kile kirefu kimezingira kijumba/kijijumba cha kijitajiri kile.
(d) Kidege/kijidege kinalisha vijikinda vyake.
(e) Vijishuka hivi vitatumika kutandika kijitanda cha kitoto/kijitoto.
5. *Tumia hali ya udogo ya nomino kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

### Zoezi la Marudio 5

1.

| Wastani | ukubwa | udogo |
|---|---|---|
| Chuma | **jichuma** | **kijichuma** |
| **Medali** | jimedali | **kijimedali** |
| **Pete** | jipete | **kijipete** |

| | | |
|---|---|---|
| **Shanga** | **jishanga** | kijishanga |
| **Mpira** | **jipira** | kijipira |
| Yai | **jiyai** | **kijiyai** |

2. (a) Jizi/Jijizi lile lilinaswa jana.
(b) Kijiatu changu kilinunuliwa kwa kijiduka hiki.
(c) Mti wa maparachichi umekatwa.
(d) Vijipesa vya kijitajiri kile vimewekwa kwa vijibenki.
(e) Jibuyu la Mwajuma ni jeupe.

# 4. Mnyambuliko wa Vitenzi

## I. Kauli ya kutenda

### Zoezi la 1

1. (a) Mwanariadha ameruka kiunzi.

(b) Ndege ametua juu ya mti.

(c) Dada anashona kitambaa cheupe.

(d) Ninataka kupika viazi.

(e) Lola anamsaidia baba kubeba mizigo.

(f) Twendeni tukazuru mbuga ya wanyama.

2. **Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Fundi anashona kiatu.

(b) Wanafunzi wanasoma vitabu.

(c) Mpishi anapika pilau.

(d) Kaka anatafuna muwa.

(e) Konokono anatembea polepole.

3. (a) Sulwe anamsaidia Jefwa kuvuna mahindi na Jefwa anamsaidia Sulwe kuvuna mahindi.

(b) Mwadime amepika chakula kwa niaba ya Omari. /Mwadime amepika chakula kwa ajili ya Omari.

(c) Maradhi yanamsumbua mgonjwa.

(d) Fundi ameshona nguo ya mama.

(e) Mchezaji anapiga mpira umwendee mwenzake/ Mchezaji anapiga mpira kwa niaba ya mwenzake.

(f) Mjomba alilipa karo kwa niaba ya Kudate.

(g) Mlinzi amefunga mlango mbwa asitoke.

(h) Wenyeji wanawashangilia wageni.

(i) Mtoto ataokota majani.

(j) Mhazili <u>atachapa</u> kitabu.

4. (a) Kasmu *alikimbia* akaingia jumbani.

(b) Wajukuu wangu *wanacheza* uwanjani.

(c) Muuguzi *amemdunga* majeruhi sindano.

(d) Swara *anatembea* mbugani.

(e) Maji *yamejaa* bwawani.

(f) Mwanahabari *anasoma* habari hizo.

(g) Mwashi aliahidi *kujenga* nyumba hiyo.

(h) Wateja *walimlipa* muuzaji kwa hundi.

(i) *Weka* kifaa hiki mezani.

(j) Ndovu *amekunywa* maji mengi.

### Zoezi la 2

1. (a) Askari walimfungia mhalifu ndani ya seli.

(b) Mkulima alilimia jembetezo badala ya trekta.

(c) Salano amemsomea Barike aya nzima.

(d) Rono amemletea Waithera kalamu na daftari.

(e) Alitaka kujua aliyewahi kutembelea Ziwa Baringo.

2. **Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Kaka ameniletea zawadi.

(b) Paulo amechimbia bibi muhogo.

(c) Tarishi aliwapelekea barua.

(d) Juma ananifungulia ndama

(e) Kazungu atamtekea Kiboi maji.

3. (a) Himidi anamwendeshea Hidaya gari.

(b) Chungu cha mama kimevunjikia mlangoni.

(c) Abiria alipandia basi kituoni.

(d) Mutua alimnunulia Wakesho mananasi.

(e) Guyo anampelekea chifu barua.

(f) Watalii walitembelea nchi ya Kenya.

(g) Alijifunzia maadili ya taifa darasani.

(h) Aliwazia jambo hilo akiwa peke yake.

(i) Alimjengea paka aliyemwokota nyumba.

(j) Nampendea Mueni ukarimu wake.

4. (a) Wachezaji *wamevalia* sare uwanjani.

(b) Watoto *wanamchezea* mbwa wao.

(c) Wanakijiji *watamjengea* mzee maskini nyumba.

(d) Samson *amemchukulia* Amina karatasi kutoka kwa mwalimu.

(e) Waumini *waliwafanyia* mchango waathiriwa wa mkasa wa moto.

(f) Mama *amempikia* mgeni biriani.

(g) Dobi *atatufulia* nguo zetu kesho.

(h) Yaya *alimlelea* mtoto wake kijijini.

(i) Shangazi *atanipokelea* mgeni wangu.

(j) Ben *amemsafishia* mamake nyumba iliyokuwa chafu.

## Zoezi la 3

1. (a) Miti hiyo ikikatwa, wahusika watatiwa mbaroni.

(b) Taka zimetupwa jaani.

(c) Mimea iling'olewa na kimbunga.

(d) Shamba lote limelimwa.

(e) Deni hilo litalipwa kwa miaka thelathini.

(f) Ukisongwa na mawazo, zungumza na mshauri nasaha.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Mbuzi amefungwa na Kantai.

(b) Wimbo  mtamu umeimbwa na Jadolo.

(c) Wageni wamepelekwa nyumbani.

(d) Chumba kitafagiliwa na watoto.

(e) Sadaka imetolewa na waumini.

3. (a) Muwa umekatwa kwa kisu.

(b) Kitabu kitasomwa na Mila.

(c) Fulana imeshonwa na dada.

(d) Maziwa yote yamenywewa na paka.

(e) Gari liliendeshwa kwa kasi kubwa na dereva.

(f) Wanyama wengi wa pori waliathiriwa na kiangazi.

(g) Bidhaa zaidi zimeagizwa na mfanyibiashara.

(h) Bidhaa hizo zitalipiwa kwa pesa taslimu.

(i) Rinda zuri limevaliwa na Amina.

(j) Mgonjwa ametibiwa ng'ambo.

**Zoezi la Marudio 6**

(a) Mvua ilinyeshea nguo zilizokuwa zimeanikwa.

(b) Ukitembea bila viatu utadungwa na mwiba.

(c) Mama ameuza viatu vyote.

(d) Duru anaonekana amesongwa na mawazo.

(e) Mvuvi alivua_ samaki wengi.

(f) Hicho kitabu ni cha kuandikia insha.

(g) Endelea kuomba, Mungu atakubali dua lako.

(h) Fundi alimtobolea tundu za kuweka vifungo vya shati.

(i) Wairimu <u>alinishikia</u> kipazasauti nilipokuwa nikitoa hotuba.

(j) Mpira <u>ulichezwa</u> ugani Kasarani.

### Zoezi la 4

1. (a) Puto lililonunuliwa na shangazi limenyumbuka.

(b) Jumba limejengeka haraka.

(c) Maswali mengi yaliibuka katika mdahalo huo.

(d) Maandishi yamefutika kwenye kitabu hicho.

(e) Maji yaliyokuwa kwenye kikombe yamemwagika

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Mlango umefunguka.

(b) Msitu wote umechomeka.

(c) Tarakilishi yake imefungika baada ya kubonyezwa.

(d) Safari yetu itakamilika kesho.

(e) Kiti cha mtoto kimevunjika.

3. (a) Mbwa alipomwona Bruno aliupigapiga mkia wake.

(b) Nyama imeiva na unaweza kuitafuna kwa urahisi.

(c) Mchele unapepetwa kwenye ungo.

(d) Mnazi huo una pandio kwa hivyo unapandwa kwa urahisi.

(e) Mkanju wa jirani ulivunjwa wakati wa dhoruba.

(f) Kigari cha mtoto kimeharibiwa.

(g) Nguo ya yatima iliyoraruliwa ilishonwa na mzazi mwenye huruma.

(h) Makubwa hayo utayanena kweli?

(i) Ndago ziling'olewa zilipovutwa kwa nguvu.

(j) Alishawishiwa kuandamana na rafiki yake kwenda kwao.

4. (a) Udongo huo <u>unalimika</u> kwa urahisi.

(b) Bidhaa <u>zimenunulika</u> kwa bei nafuu.

(c) Tarakilishi ya Hawi <u>imeharibika</u> hivyo hawezi kuitumia.

(d) Kiti cha Beja ni kizito hivyo <u>hakitabebeka</u> na mtoto mdogo.

(e) Hiyo kazi ilikuwa ngumu ila hatimaye <u>ilimalizika</u>.

(f) Ukifika karibu na mti mkubwa <u>pinduka</u> mkono wa kushoto na utaona nyumba yetu.

(g) Mlango <u>ulifunguka</u> wenyewe tukaingia ndani.

(h) Njia hiyo ni nzuri hivyo <u>itapitika</u> vyema.

(i) Unafikiri vitabu vilivyonunuliwa <u>vitasomeka</u>?

(j) Mtu huyo <u>anafahamika</u> sana humu nchini.

**Zoezi la 5**

1. (a) Ng'ombe amekatiwa majani na mkulima.

(b) Mwana wa Hagari alichotewa maji na jirani.

(c) Maino alishindiwa uwanja wa Mashujaa.

(d) Ibu alipikiwa biriani kwenye sufuria kubwa.

(e) Waimbaji watapokelewa wageni wao kituoni.

(f) Mkurugenzi alichukuliwa barua na tarishi.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Ereng' amelipiwa nauli na dereva.

(b) Maore amepikiwa uji na mamake.

(c) Mtoto amefungiwa kiwinda na mlezi.

(d) Yeye atavumbikiwa ndizi na muuzaji.

(e) Mtoto ameandaliwa matobosha na nyanyake.

3. (a) Alivutiwa gari kutoka lilikokwamia.

(b) Mkulima anafyekewa nyasi.

(c) Kisima kilichimbiwa jangwani.

(d) Mtoto alikatiwa hindi la kuchoma na mama.

(e) Watoto <u>wamepikiwa</u> chapati na kijakazi.

(f) Tawi linatembelewa na mdudu.

(g) Kina mama wameuziwa dagaa na mvuvi.

(h) Ukuta unatambaliwa na tandu.

(i) Reli ilijengewa wachukuzi wasafirishe mizigo yao.

(j) Mpishi amenolewa kisu na mjumu.

4. (a) Wanafunzi <u>wanasahihishiwa</u> vitabu na mwalimu.

(b) Mwashi <u>alibebewa</u> simiti kwa toroli na Omollo.

(c) Noah <u>alishindiwa</u> shindano hilo na Tebago.

(d) Mache <u>amekaririwa</u> shairi na mwanafunzi.

(e) Sangale <u>amepandiwa</u> miche shambani mwake na Kande.

(f) Mtoto <u>alifuliwa</u> nguo na dobi.

(g) Kikaango <u>kimeepuliwa</u> motoni na Mumina.

(h) Mhalifu <u>alizuiliwa</u> langoni na askari.

(i) Huwezi <u>kuumbuliwa</u> na asiyeweza kukuumba.

(j) Karatasi iliyokuwa ukutani <u>imebanduliwa</u> na Ali.

**Zoezi la 6**

1. (a) Maji yaliyojaa bilauri yanamwagikamwagika.

(b) Mbona unaigongagonga sakafu kwa mkongojo?

(c) Esta aliokotaokota mashuke ya ngano kutoka shambani.

(d) Gangaganga za mganga humpa mgonjwa matumaini.

(e) Baada ya kushikashika maembe hayo, alichagua mawili tu.

(f) Njiwa anadonadona punje za mtama.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Mkurugenzi anapigapiga simu ofisini.

(b) Zuena anapekuapekua faili.

(c) Adili anachumachuma maua kondeni.

(d) Mishi anabofyabofya parachichi.

(e) Watoto wanachezacheza barazani.

3. (a) Mbungu hupitapita hapa.

(b) Mtoto mgonjwa hulialia.

(c) Nyani ameumauma ndizi iliyokuwa kikapuni.

(d) Haifai kumpigapiga mnyama yeyote.

(e) Akitembea hukanyagakanyaga kanzu yake.

(f) Bashasha huchekacheka sana.

(g) Kiongozi huyo hubanduliwabanduliwa mamlakani katika kila kikao.

(h) Mbona unaandikaandika ubaoni ukifutafuta?

(i) Ndege wanaimbaimba viotani.

(j) Mbwa wanabwekabweka sana leo, sijui kwa nini.

4. (a) Mgonjwa anachaguachagua chakula.

(b) Lofa anazururazurura mtaani, hana kazi wala bazi.

(c) Hufai kumwitaita mwenzako bila sababu.

(d) Walipozuru Uturuki walinunuanunua vyombo.

(e) Malizeni shughuli mapema, mkiendelea kuzembeazembea hamtakamilisha.

(f) Tutajaribujaribu mpaka tufaulu.

(g) Mvua inanyeshanyesha tangu jana.

(h) Wahasiriwa walihamahama hadi wakapata makao mapya.

(i) Endeleeni kusomasoma mpaka muelewe.

(j) Alitafutatafuta hatimaye akapata suluhisho.

## Zoezi la Marudio 7

1 (a) Huonyesha kuwa kitendo kimefanyika bila kusababishwa au bila kumtaja mtendaji

(b) Huonyesha kuwa kitendo kimefanywa kwa niaba ya mtu mwingine au kwa ajili ya mtu mwingine.

(c) Huonyesha kurudiarudia kitendo.

2. (a) zoleka, zibika, tembeleka

(b) mwagiwa, somewa, andikiwa

(c) tafunatafuna, kunakuna, gonganga

3. (a) (i) Taka zote <u>zilizoleka</u> kwa urahisi.

(ii) Bomba la maji <u>limezibika</u> hata baada ya fundi kulikarabati.

(iii) Njia hiyo <u>inatembeleka</u> kwa urahisi.

(b) (i) Ukipita karibu na baraza lake <u>utamwagiwa</u> maji kwani panavuja.

(ii) <u>Mtasomewa</u> masharti yote kabla ya kuanza shughuli hiyo.

(iii) Magati <u>aliandikiwa</u> barua na rafiki yake.

(c) (i) Mbona <u>unatafunatafuna</u> maneno? Yatamke vizuri!

(ii) Nayiyoma <u>anajikunakuna</u> kwa vile ametambaliwa na mdudu.

(iii) Kimoli <u>anagongagonga</u> mlango kwa chuma.

4.

| Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendewa | Kauli ya kutendatenda |
|---|---|---|
| wametawanyika<br>kusaidika<br>huburudika<br>kuchangamka<br>kutamanika<br>kupendeka | kufanyiwa<br>husaidiwa<br>kubebewa<br>huletewa<br>hulindiwa<br>hununuliwa | wakiimbaimba<br>huchezacheza<br>kurukaruka<br>wanaopitapita<br>wakiuzauza |

5. *Kitungwe kifungu kifupi kuhusu haki za watoto. Kifungu hicho kizingatie matumizi ya vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda.*

**Zoezi la 7**

(a) Watu katika jamii ile wanapendana sana.

(b) Tulionana naye mjini.

(c) Tutakutana majaliwa.

(d) Sijui mbona wanapingana ilhali jambo hilo ni wazi kabisa.

(e) Walishauriwa waache kugombana kwa kuwa amani ni muhimu.

(f) Zuena na Nafula wanaandikana mikono kwa kalamu nyekundu.

(g) Mkipigana mtaumizana bure.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Marafiki hao walilipana madeni yao.

(b) Wanyama walikanyagana mbugani.

(c) Wanasarakasi walipakana rangi kwenye nyuso zao.

(d) Askari walifyatuliana risasi na majambazi.

(e) Watoto wakiachiwa wembe wachezee, watakatana.

3. (a) Mkulima na mwanawe <u>wamevuniana</u> nafaka.

(b) Sambu na Hakim <u>wanachekana</u>.

(c) Gijo na Habona <u>wanasubiriana</u>.

(d) Koech na Wekesa <u>wamerushiana</u> mpira.

(e) Maria na dada yake walibebana.

(f) <u>Tutaonana</u>.

(g) <u>Tukisaidiana</u> tutafikia kilele cha ufanisi.

(h) Wananchi na kiongozi <u>wanaheshimiana</u>.

(i) Wakubwa na wadogo <u>wanalaumiana</u>.

(j) Mama na mwanawe <u>wanapendana</u>.

4. (a) Radhia na Mashaka <u>wanasaidiana</u> kufanya kazi.

(b) Majirani hao <u>huzozana</u> siku zote.

(c) Tangu <u>wapatane</u>, hawatengani kamwe.

(d) Walipopewa zawadi, mahafala hao <u>walishangiliana</u>.

(e) Kuna haja gani <u>kugombana</u>? Ishini kwa amani.

(f) <u>Waliliwazana</u> kwa nyimbo za kutuliza nyoyo.

(g) Majembe yakiwekwa pamoja hayakosi <u>kugongana</u>.

(h) Japo tumetengana hatuachi <u>kushirikiana</u>.

(i) Mabondia <u>walipigana</u> ngumi kwa kasi wakati wa mchuano.

(j) Wasusi hawana wateja kwa hivyo <u>wanasongana</u> wenyewe.

**Zoezi la 8**

1. (a) Raha na Aska wanachimbiana mashimo kwenye mashamba yao.

(b) Walilipiana madeni kwa kuwa walikuwa marafiki.

(c) Mahamali walipakiana mizigo bandarini.

(d) Mhubiri alitufunza umuhimu wa kuombeana.

(e) Marafiki hao hupenda kupikiana vyakula vya kila aina.

(f) Wao huchezeana kila mara bila kukosana.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Tulinunuliana zawadi wakati wa tamasha hizo.

(b) Zena na Malebo waliamkuana wakati wa likizo.

(c) Shule zilipofungwa wazazi walishauriana kuhusu wana wao.

(d) Wauzaji sokoni waliuziana bidhaa zao.

(e) Maprofesa walivuliana kofia kwa heshima walipokutana.

3. (a) Zari na Lutaya walilipiana nauli.

(b) Tulisameheana.

(c) Chebet na Kahura walipigiana simu.

(d) Gari la abiria na la mizigo yalingojeana ili yavuke mpaka pamoja.

(e) Atur na Akoth walifagiliana vyumba vyao.

(f) Tulitumiana salamu.

(g) Tulipakiana kucha rangi na Sara.

(h) Emili na Rozi walitembeleana.

(i) Jimi na Rosana waliandikiana barua.

(j) Mbuvi na Nyaboke wanaimbiana nyimbo tamu.

4. (a) Wakimbizi walibebeana mizigo walipotoka kambini.

(b) Tutatambiana hadithi kabla ya kuandika insha.

(c) Kina mama wanauziana mahindi sokoni.

(d) Wakulima watalimiana mashamba yao.

(e) Washenga watapelekeana posa.

(f) Marafiki wema walitimiziana/hutimiziana ahadi zao.

(g) Wanafunzi walifuliana mashati yao.

(h) Walisimama kwenye foleni na kupokeana zawadi.

(i) Wanakijiji walijengeana nyumba kwa ujima.

(j) Walipokosana walishtakiana kortini.

## Zoezi la 9

1. (a) Kocha alichezesha timu yetu mpira.

(b) Tembo amepigisha mkonga wake kwenye mti.

(c) Mwalimu anamsomesha mwanafunzi.

(d) Baada ya rais kupanda mti, Petero alimnavya mikono kwa maji safi na sabuni.

(e) Ukuta uliopakwa rangi unapendeza.

### 2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:

(a) Aligongesha kichwa chake dirishani kwa bahati mbaya.

(b) Pitisha kitabu hicho mpaka kimfikie mwalimu.

(c) Anzisha mkutano, muda unayoyoma!

(d) Zungusha uzi huo kwenye sindano ili isipotee.

(e) Utamkaribisha mgeni akifika.

3. (a) Yaya anamtembeza mtoto.

(b) Uongozi umemlevya hivyo hamheshimu yeyote.

(c) Mbwa wa jirani walimkimbiza mpaka kwao.

(d) Tulitozwa ushuru bidhaa zote tulizokuwa tumebeba.

(e) Dada amempikisha mdogo wake.

(f) Wanasarakasi waliigiza mchezo jukwaani.

(g) Aliinua mkono na kulisimamisha basi.

(h) Nyasi walizokula zimewashibisha faru na mbogo.

(i) Maji safi yalimtakasa mwili mzima.

(j) Ng'ombe anamnyonyesha ndama wake.

4. (a) walibomoza (b) kiliwakasirisha (c) wakiendesha

(d) walisitisha (e) yakiwashughulisha (f) kusomesha/kufundisha

(g) akiwachezasha (h) kusalimisha (i) kushtusha

(j) kuwaogopesha/kuwaogofya (k) kulisimamisha

(l) akajisogeza (m) Alijifikisha (n) wangelipisha

(o) liliwafurahisha

## Zoezi la Marudio 8

1. (a) Kauli ya kutendana huonyesha wahusika wakielekezana kitendo hicho hicho.

(b) Kauli ya kutendeana ni muungano wa kutendea na kutendana ambapo mhusika hutenda kwa niaba ya mtu mwingine.

(c) Kauli ya kutendesha huonyesha kuwa mtu au hali imesababisha kitendo kufanyika.

2. (a) shikana, taniana, kosana

(b) liliana, ondoleana, jengeana

(c) elewesha, simamisha,chemsha

3. (a) (i) Watoto wameshikana mikono watengeneze duara.

(ii) Yuni na Sofi hupenda kutaniana.

(iii) Kalume na Sombe walikosana ila Saruni aliwapatanisha.

(b) (i) Marafiki walililiana mmoja wao alipohamia ughaibuni.

(ii) Tulipoelewana, tuliondoleana lawama.

(iii) Tutajengeana majumba ya bei nafuu.

(c) (i) Mwalimu alimweleza taratibu na hatimaye kumwelewesha mada hiyo.

(ii) Simamisha mkeka huo chini ya mti ule.

(iii) Chemsha viazi kisha uviponde.

4. (a) pendana

(b) hubebeana

(c) shikana

(d) humbebesha

(e) huwavusha

(f) pungiana

(g) heshimiana

(h) saidiana

(i) andamana

(j) zoeana

(k) tembeleana

(l) nadhifisha

(m) takasa

(n) kosesha

# 5. Vinyume vya Maneno

## I. Nomino

### Zoezi la 1

1. ***Majibu yanayopendekezwa***

| |
|---|
| kuanza – kumaliza, tajiri – maskini, mnunuzi – muuzaji, adui – rafiki |

2. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Tuliokolewa kutoka kwa utumwa baada ya kupata uhuru.
(b) Usiku huu utakuwa mtulivu kuliko mchana tuliposhuhudia maandamano.
(c) Mfalme na malkia walihudhuria sherehe nchini mwetu.
(d) Aliwatendea wema hata baada ya ubaya alioupata.
(e) Mkutano huo ulijaa wazazi na watoto wao.

3. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Kicheko cha mwanafunzi yule asiyejali kiligeuka kilio baada ya kuadhibiwa. (*Kicheko – kilio*)
(b) Baada ya vita vya miaka mingi nchini mwao, sasa kuna amani. (*vita – amani*)
(c) Tulipanda milima na kushuka mabonde tukielekea jijini Nakuru. (*Tulipanda – kushuka*)
(d) Likizo ijayo nitawatembelea shangazi na mjomba kule Mombasa. (*shangazi – mjomba*)
(e) Binadamu wanafaa waishi kwa upendo bila chuki yoyote. (*upendo – chuki*)
(f) Joto la mwezi huu limezidi baada ya kuwa na baridi ya miezi mitatu. (*Joto – baridi*)
(g) Asubuhi hapatikani lakini jioni huwa amefungua duka lake. (*Asubuhi – jioni*)
(h) Uvivu wa Mwakuona ulisababisha ashindwe na bidii ya Mwabaya. (*Uvivu – bidii*)
(i) Alivumilia uchungu wa shubiri ili apate kuonja utamu wa asali. (*uchungu – utamu*)
(j) Kakake alimwoa dadake Samido kwa harusi kubwa. (*Kakake – dadake*)

4. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mwizi alivunja kwangu akaiba jogoo mmoja na koo watatu.
(b) Madereva wanapaswa wachunge uhai wa watu ili waepuke vifo.
(c) Nkubitu ana ujasiri, hana woga kama aliokuwa nao zamani.

5. *Tumia nomino ulizopewa kutunga sentensi sahihi.*

   Kwa mfano: Mimi ninatazama mbingu.

6. (a) *Andika kinyume cha sentensi ulizotunga katika nambari ya 5.*

   Kwa mfano: Mimi ninatazama ardhi.

   (b) *Sentensi zisambazwe kwa wengine ili wazitolee maoni.*

## II. Vivumishi

### Zoezi la 2

1.

| |
|---|
| maskini – tajiri, wadogo – wakubwa, kibaya – kizuri, mrefu – mfupi |

**2. Majibu yanayopendekezwa**:

(a) Polisi walisimamisha magari mapya na mazee ili kuyakagua. (*mapya – mazee*)
(b) Tuwe watu wakarimu kwani watu wachoyo hawapendwi. (*wakarimu – wachoyo*)
(c) Asali tamu ilipakwa kwenye mkate na pilipili chungu ikatiwa kwenye wali. (*tamu – chungu*)
(d) Wanafunzi wakubwa walisimama na wanafunzi wadogo gwarideni. (*wakubwa – wadogo*)
(e) Kuna maembe haba na machungwa tele sokoni. (*haba – tele*)

**3. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Watu wema na waovu huishi miongoni mwetu.
(b) Mkulima alinunua shoka kali lakini baada ya mwezi mmoja likawa butu.
(c) Watoto wakaidi hawapendwi kama watoto watiifu.
(d) Barabara nyembamba ya kwetu ilitumika na lori pana la kubeba mchanga.
(e) Mtoto alikataa kula mkate mgumu mpaka akatafutiwa ule laini.

**4. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mkulima mzee alimuuzia mwalimu kijana mboga na matunda.
(b) Miti mirefu na mifupi ilipaliliwa na wanafunzi.
(c) Tunastahili kumshukuru Mungu kwa neema kubwa na ndogo.
(d) Vigingi vyepesi vilibebwa pamoja na vile vizito.

5. *Tumia vivumishi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi.* Kwa mfano:Mwanafunzi amesoma vitabu vichache.
6. (a) *Andika kinyume cha sentensi ulizotunga katika nambari ya 5.* Kwa mfano: Mwanafunzi amesoma vitabu vingi.
   (b) *Sentensi zisambazwe kwa wengine ili wazitolee maoni.*

### III. Vitenzi

### Zoezi la 3

**1. Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| keti – simama, pata – kosa, tia – toa, anika – anua, vaa – vua |

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Baada ya kukataa kunitembelea, alikubali nilipombembeleza. (*kukataa – alikubali*)

(b) Baba aliziba shimo la panya naye mbwa akalizibua. (*aliziba – akalizibua*)

(c) Alifunika chupa ya maziwa naye mtoto akaifunua. (*Alifunika – akaifunua*)

(d) Mkeka ule ulitandikwa asubuhi ili ukauke na kutanduliwa jioni. (*ulitandikwa – kutanduliwa*)

(e) Asiyeweza kukuumba hawezi kukuumbua. (*kukuumba – kukuumbua*)

**3. Majibu yanayopendekezwa**

(a) Marimba alichota maji na kuyamwaga kwenye maua.

(b) Ukienda mjini kesho hakikisha kwamba utarudi mapema.

(c) Mbwa yule alimeza nyama kwa ulafi lakini akazitema aliponyongwa.

(d) Sisi hulala saa tano usiku na kuamka saa kumi alfajiri.

(e) Tusiwe tunanuna kila wakati bali tuwe tunatabasamu.

(f) Wakristo walifumba macho na kuyafumbua baada ya maombi.

(g) Wananchi walikusanyika wakahutubiwa na mwanasiasa kisha wakatawanyika.

(h) Nyanyangu alinitegea kitendawili nami nikashindwa kukitegua.

(i) Ukipewa siri ili uifiche haufai kuifichua.

(j) Josie alifuma fulana ya mtoto lakini ilipoharibika akaifumua.

**4. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mwalimu aliwakosoa wanafunzi waliokosa kwa kupiga kelele darasani.

(b) Mizigo iliyopakiwa ndani ya lori ilipakuliwa na wanaume watano.

(c) Usipooga utanuka kama beberu lakini ukioga utanukia.

(d) Mutea alikunjua nguo alizokuwa amezikunja alipozinunua dukani.

5. Tumia vitenzi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi. Kwa mfano: Wafanyakazi wote wameinama.
6. (a) *Andika vinyume vya sentensi ulizotunga katika nambari ya 5.* Kwa mfano: Wafanyakazi wote wameinuka.

(b) *Sentesi zisanbazwe kwa wengine ili wazitolee maoni.*

## IV. Vielezi

### Zoezi la 4

1. **Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| magharibi – mashariki, ndani – nje, nyingi – chache, mnene – mwembamba, mwanzoni – mwishoni, vizuri – vibaya |

2. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Tulianza kazi hiyo asubuhi na tunatarajia kuimaliza jioni. (*asubuhi – jioni*)

(b) Barabara hii ni mbaya. Itarekebishwa wiki ijayo ili iwe nzuri. (*mbaya – nzuri*)

(c) Jua huchomoza upande wa Mashariki na kutua upande wa Magharibi. (*Mashariki – Magharibi*)

(d) Ukipanda sehemu iliyo juu utaona nyumba zote zilizo huku chini. (*juu – chini*)

(e) Waliofika walikuwa wengi lakini waliopata chakula walikuwa wachache. (*wengi – wachache*)

3. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mbona uliendesha pikipiki <u>harakaharaka</u> na nilikwambia uiendeshe <u>polepole</u>?

(b) Omondi alivua samaki <u>usiku kucha</u> kisha akalala <u>mchana kutwa</u>.

(c) Nilisafiri nikafika <u>kabla</u> yake naye akafika <u>baadaye</u> kidogo.

(d) Tulisimama <u>nje</u> kwa muda na baadaye tukaitwa <u>ndani</u>.

(e) Nilimwona mfalme kwa mara ya <u>kwanza</u> na mara ya <u>mwisho</u> miaka mitano iliyopita.

4. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Ukifika mbele mweleze kuwa wengine watafika nyuma.

(b) Mchezaji alilazwa kifudifudi uwanjani baada ya kulala chali kwa muda.

(c) Biashara ya Kiambati ni ya kununua kwa jumla na kuuza rejareja.

(d) Sare yake ya shule ilikuwa chafu na alipoifua ikawa safi.

5. Tumia vielezi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi. Kwa mfano: Mama aliondoka jioni.

6. (a) Andika vinyume vya sentensi ulizotunga katika nambari ya 5. Kwa mfano: Mama aliondoka asubuhi.

   (b) Sentensi zisambazwe kwa wengine ili wazitolee maoni.

## V. Vihusishi

### Zoezi la 5

1. **Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| baada ya – kabla ya,  juu ya – chini ya, mbele ya – nyuma ya |

2. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mwanafunzi mmoja amesimama mbele ya darasa na wengine nyuma ya bweni. (*mbele ya – nyuma ya*)

(b) Mashabiki waliosimama karibu na wachezaji waliagizwa wasimame mbali na wachezaji hao. (*karibu na - mbali na*)

(c) Upepo mkali ulitoka mashariki mwa ziwa na kuelekea magharibi mwa nchi. (*mashariki mwa – magharibi mwa*)

(d) Aliitafuta kalamu juu ya kabati na kuangalia chini ya kabati lakini hakuipata. (*juu ya – chini ya*)

(e) Kangai alitoka baada ya mamake kuondoka na akarudi kabla ya kurejea kwake. *(baada ya – kabla ya*)

3. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Watoto walijificha <u>ndani ya</u> maua walipokuwa wakicheza <u>nje ya</u> nyumba.

(b) Aliegesha gari <u>karibu na</u> lango lililokuwa <u>mbali na</u> sehemu ya mkutano.

(c) Ukifanya mtihani <u>bila ya</u> makini utaibuka <u>ukiwa na</u> gredi duni.

(d) Mbegu zilizopandwa <u>kabla ya</u> mvua kunyesha zilimea <u>baada ya</u> siku tatu.

(e) Dereva alitoka <u>mbele ya</u> gari akasimama <u>nyuma ya</u> abiria walioliabiri.

(f) Chui alipanda <u>juu ya</u> mti naye simba akapita <u>chini ya</u> mti huo.

4. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Wimbo ulichezwa baada ya taarifa ya habari.

(b) Kwetu ni magharibi mwa mji wa Meru.

(c) Alisimama kandokando ya umati wa watu.

(d) Kadogo aliendesha baiskeli yake mbali na barabara.

5. *Tumia vihusishi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi*. Kwa mfano: Mtoto alijificha chini ya kitanda.

6. (a) *Andika vinyume vya sentensi ulizotunga katika nambari ya 5*. Kwa mfano: Mtoto alijificha juu ya kitanda.

(b) *Sentensi zisambazwe kwa wengine ili wazitolee maoni.*

## Zoezi la Marudio 9

### Majibu yanayopendekezwa:

1. (b)

| | **Nomino na vinyume vyao** | **Vivumishi na vinyume vyao** |
|---|---|---|
| (i) | jioni – asubuhi | mpya – nzee |
| (ii) | wakubwa – wadogo | chache - nyingi |
| (iii) | wanaume – wanawake | safi – chafu |
| (iv) | wafalme – malkia | |

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Kulipa kwa watu wengine huwa kazi ngumu.

(b) Mtu mkweli akiongea utamjua tu.

(c) Nyumba ile ilijengwa kwa msingi imara.

(d) Ufupi wake ulimfanya atambulike haraka.

(e) Afya ya ng'ombe yule inafaa iangaliwe.

(f) Mzigo mzito uliwekwa ndani ya lori.

(g) Joto la maji hayo lilinifanya nishindwe kuyanywa.

(h) Bidii yako inakufanya usipendwe na wenzako.

(i) Shati lile jeusi limechafuka.

(j) Wezi walitumia kisu kikali kumshambulia.

**3. (b) Majibu yanayopendekezwa:**

| | **Vitenzi na vinyume vyao** | **Vielezi na vinyume vyao** |
|---|---|---|
| (i) | huamka – hulala | asubuhi – jioni |
| (ii) | hupata – hukosa | mchana kutwa – usiku kucha |

| | | |
|---|---|---|
| (iii) | wanapofurahia – wanahuzunikia | mara nyingi – mara chache |
| (iv) | wanakonunuliwa – huuzia | rejareja – jumla |

**4. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Ukitia bidii na upate kufanikiwa leo, jizatiti zaidi.

(b) Ole Tip Tip alimchomoa ng'ombe mshale ili apate damu.

(c) Tutatoka shambani asubuhi.

(d) Mgeni mheshimiwa atawazungumzia mwanzoni.

(e) Anua nguo ulizofua kabla mvua inyeshe.

(f) Tulifanya mazoezi ya kushuka chini mlimani.

(g) Kwaya iliimba wimbo kwa huzuni.

(h) Wanasiasa walitembelea eneo la Mashariki.

(i) "Simameni mara moja!" mwalimu alituamrisha.

(j) Nimetoa pesa zangu mfukoni.

# 6. Nyakati na Hali

## (a) Wakati uliopo

### Zoezi la 1

1. ninapika, kinapikwa, inakolea, anatambua

2. (a) inashiriki (b) Panaendelea (c) zinatengenezwa (d) inanywewa (e) kinashonwa

3. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika wakati uliopo kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

(b) Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(i) Swara anakimbia. (ii) Wanafunzi wanafurahi. (iii) Watahiniwa wote wanafuzu. (iv) Huyu anawakilisha eneobunge letu. (v) Mgeni anapotea njia.

## (b) Wakati uliopita

### Zoezi la 2

1. (a) zilifunguliwa (b) yalinadhifishwa (c) alishinda (d) alizuru (e) ulikuwa

2. (a) Begi lilibebwa na mwanafunzi.

(b) Pesa nyingi zilikuwa za muuzaji.

(c) Nyanya alienda safari ndefu.

3. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika wakati uliopita kutunga sentensi sahihi kisarufi*.

(b) Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(i) Kala aliamka asubuhi sana. (ii) Sote tulisali leo. (iii) Mboga ziliuzwa sokoni. (iv) Sote tulikunywa maziwa. (v) Mashabiki walishangilia.

4. (a) (i) zilivaliwa (ii) palioshwa (iii) vilipikwa (iv) alishona (v) aliandika

(b) (i) Seremala alilainisha mbao. (ii) Uji ulipikwa na babu. (iii) Kitanda kilitandikwa. (iv) Suti ililainishwa kwa pasi. (v) Umati ulishangilia wanariadha.

## (c) Wakati ujao

### Zoezi la 3

1. watasakura, kitafura, wataoka, litaliwa

2. (a) (i) mtamkaribisha (ii) itasakifiwa (iii) watalitazama (iv) kutapendeza

(b) Itakuwa siku ya Jumapili. Anyango ataamka asubuhi na mapema. Atatandika kitanda na kuingia bafuni kuoga. Atavaa nguo nzuri ambayo babake atamnunulia. Atachana nywele zake

ambazo zitakuwa ndefu kupindukia. Atakunywa uji ambao Ali ataupika. Baada ya hapo, ataenda kanisani. Atajiunga na waumini wengine kusali.

3. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika wakati ujao kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

(b) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika wakati ujao kutunga kifungu cha aya moja kuhusu unyanyasaji wa kijinsia.*

## Zoezi la Marudio 10

1. Jaza jedwali ifuatavyo.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita | Wakati ujao |
|---|---|---|
| Inaendelea | Waliteuliwa | atashinda |
| Inapeperushwa | Walishiriki | watatazama |
| Inawakilishwa | | Watamshangilia |
| Wanatarajiwa | | |
| Tunamwamini | | |
| Tunatumai | | |

2. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika wakati uliopo kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

(b) *Zibadilishe sentensi ulizozitunga katika 2(a) ziwe katika wakati uliopita*.

(c) *Zibadilishe sentensi ulizozitunga katika 2(a) ziwe katika wakati ujao*.

3. Michezo ya olimpiki iliendelea na ilipeperushwa moja kwa moja kwenye televisheni. Nchi yetu iliwakilishwa na wanariadha wengi. Wanariadha hawa waliteuliwa baada ya ushindi wao wakati walishiriki katika mbio za mchujo nchini. Miongoni mwa wale ambao walitarajiwa kushinda medali ni Omanyala. Tulimwamini sana mwanariadha huyu. Tulitumai kuwa angeshinda mbio za mita mia moja. Wananchi wengi walitazama mbio hizi kwenye televisheni. Walimshangilia sana.

## Hali

### (a) Hali ya mazoea

### Zoezi la 1

1. hutibu, hupikwa, huchota

2. Pigia mstari vitenzi vifuatavyo.

(a) hununua (b) hufunguliwa (c) hunukia (d) hutumika (e) huoshwa, hufunguliwa

3. (a) huuzwa (b) hufunzwa (c) huendesha (d) huzimwa (e) huimbwa

4. *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika hali ya mazoea kutunga sentensi sahihi kisarufi*.

### (b) Hali timilifu

### Zoezi la 2

1. wamehamasishwa, Wameelewa, yamenadhifishwa, Wameng'amua, imenunuliwa, Wameshirikiana, kimepokea, wamekuja, Tumeshuhudia, wameahidi

2. (a) amefuzu (b) yametundwa (c) kimejaa (d) imeharibika (e) wamesakura

3. *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo katika hali timilifu kutunga sentensi sahihi kisarufi*.

### (c) Hali ya -ka- ya kufuatana kwa vitendo

### Zoezi la 3

1. akapekua, akakata, vikashonwa, ikakamatwa

2. (a) Waziri aliulizwa maswali akajitetea.

(b) Kichwa kilimwanga, akaenda hospitalini na akatibiwa.

(c) Nywele zilioshwa kisha zikasukwa.

(d) Sanduku lilitengenezwa na likawekwa nguo.

3. Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(a) Mashabiki walishangilia, timu ikashinda na wakafurahi.

(b) Alinunua kitabu, akalipa kisha akarudi nyumbani.

(c) Alilima, akapanda, akapalilia kisha akavuna.

(d) Mama alikata kitunguu, akakaanga chakula, akatupakulia na tukala.

### (d) Hali ya masharti

### (i) -ki- ya masharti

### Zoezi la 4

1. (a) Akipewa (b) tukifanya (c) wakiwa (d) ikitengenezwa (e) ukigongwa

2. (a) Miswaki mipya ikinunuliwa watoto wataitumia.

(b) Bei ya bidhaa ikishuka watu watazinunua kwa wingi.

(c) Mafuta yakinunuliwa Omolo atapika chapati..

3. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo na -ki- ya masharti kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

(b) Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(i) Mgeni akifika nitamlaki.

(ii) Yaya akiosha nguo hii mtoto ataivaa.

(iii) Ukimakinika utaelewa.

(iv) Duma akiwinda atamkamata swara.

(v) Mkulima akifuga nguruwe atawauza kwa soko hili.

### (ii) -nge- ya masharti

### Zoezi la 5

1. (a) Maziwa yangekuwa mengi chai ingepikwa.

(b) Kushona kungekamilika nguo hizo zingevaliwa leo.

(c) Dawa ingewekwa karibu watoto wangeifikia.

2. (a) Kipindi kingeisha watoto wangeenda kulala.

(b) Simu zingenunuliwa mawasiliano yangerahisishwa.

3. (a) Ningekuwa na leso ningejifunga.

(b) Nywele zingesukwa zingekuwa nadhifu.

(c) Mwanariadha angekimbia kwa kasi angeshinda mbio hizo.

(d) Sherehe ingeandaliwa watu wengi wangehudhuria.

(e) Kipakatalishi kingekuwapo wanafunzi wangesakura mtandaoni.

4. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo na -nge- ya masharti kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

(b) Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(i) Tungepika tungekula.

(ii) Wangeenda wangemkuta.

(iii) Kiatu kingenunuliwa ningekivaa.

(iv) Wanafunzi wangesoma novella hiyo wangefurahia.

(v) Kidonda kingetibiwa kingepona.

### (iii) -ngali- ya masharti

### Zoezi la 6

1. (a) (i) Loita angalikuwa mrefu angalicheza voliboli.

(ii) Soko lingalifunguliwa ng’ombe wengi wangaliuzwa.

(iii) Vita vingalitanda chuki ingalisambaa kote.

(b) (i) Watoto wangalipata lishe bora wangalikuwa na afya njema.

(ii) Sanamu ingalichongwa vizuri watalii wangaliinunua.

2. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vilivyo na –ngali- ya masharti kutunga sentensi sahihi kisarufi*.

(b) Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.

(i) Jogoo angaliwika mama angaliamka mapema.

(ii) Kuku angaliangua vifaranga anagaliwalinda.

(iii) Mimi ningaliogelea ningalifanya mazoezi.

(iv) Misitu ingalihifadhiwa ingaliwavutia watalii.

(v) Mihogo ingalipikwa tungaliikula.

## (a) Wakati uliopita hali ya kuendelea

### Zoezi la 1

1. (a) alikuwa akilala (b) ilikuwa ikiangikwa (c) walikuwa wakiyumba (d) lilikuwa likiendelea (e) ilikuwa ikisaga

2. lilikuwa likipita, lilikuwa likiwabeba, lilikuwa likiwafikisha, walikuwa wakinunua, ilikuwa ikipanda

3. *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoashiria wakati uliopita hali ya kuendelea kutunga sentensi sahihi kisarufi*.

## (b) Wakati ujao hali ya kuendelea

### Zoezi la 2

1. (a) litakuwa likipita (b) atakuwa akitengeneza (c) watakuwa wakitutumbuiza (d) atakuwa akiwinda, watakuwa wakitoroka (e) zitakuwa zikiwafurahisha

2. watakuwa wakiizuru, watakuwa wakitoka, watakuwa wakija, watakuwa wakisafiri, Watakuwa wakizuru, watakuwa wakienda, Watakuwa wakinunua

3. *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoashiria wakati ujao hali ya kuendelea kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

## (c) Wakati uliopita hali timilifu

### Zoezi la 3

1. (a) alikuwa amepiga (b) ilikuwa imetengenezwa (c) zilikuwa zimenadhifishwa (d) kilikuwa kimejaa (e) palikuwa pametayarishwa
2. Lilikuwa limechomoza, yalikuwa yameganda, ulikuwa umenunuliwa
3. (a) ilikuwa imevaliwa/zilikuwa zimevaliwa (b) walikuwa wamelalamika (c) vilikuwa vimesikika (d) kilikuwa kimekaliwa (e) lilikuwa limejaa
4. *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoashiria wakati uliopita hali timilifu kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

## (d) Wakati ujao hali timilifu

### Zoezi la 4

1. (a) kitakuwa kimewekwa (b) watakuwa wamevuliwa (c) nitakuwa nimesafiri (d) utakuwa umemkinga (e) itakuwa imefyekwa
2. utakuwa umefungwa, litakuwa limeshonwa, zitakuwa zimeenea, utakuwa umeuzwa
3. (a) watakuwa wamelima (b) vitakuwa vimechafuka (c) utakuwa umetumika (d) atakuwa amemaliza (e) itakuwa imepigwa
4. *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoashiria wakati ujao hali timilifu kutunga sentensi sahihi kisarufi.*

## Zoezi la Marudio 11

1. (a) Sentensi ya (i) inaonyesha kuwa vitendo vinavyotegemeana havikutendeka na kuna uwezekano wa kutendeka ilhali sentensi ya (ii) inaonyesha kuwa vitendo vinavyotegemeana havikutendeka na hakuna uwezekano wa kutendeka.
(b) Sentensi ya (i) inaonyesha kuwa vitendo vinavyotegemeana havikutendeka na hakuna uwezekano wa kutendeka ilhali sentensi ya (ii) inaonyesha kuwa vitendo vinavyotegemeana havikutendeka na kuna uwezekano wa kutendeka.
2. Watalii wengi walikuwa wakiizuru nchi yetu. Watalii hawa walikuwa wakitoka ughaibuni. Wengi walikuwa wakija kujivinjari. Watalii hawa walikuwa wakisafiri kwa magari spesheli ya kutalii. Walikuwa wakizuru mbuga za wanyama na wengine walikuwa wakienda pwani mwa

nchi kuogelea baharini. Walikuwa wakinunua na kutumia raslimali za nchi yetu. Hii ilikuwa ikichangia kuimarika kwa uchumi wa nchi.

3. (a) Nyanya atakuwa ameshona nguo.

(b) Nchi ilikuwa imejinyakulia uhuru.

(c) Upepo ulikuwa umevuma sana.

(d) Wote watakuwa wameshuhudia.

(e) Nyota zitakuwa zimemetameta usiku.

(f) Tikiti lilikuwa limeliwa tayari.

# 7. Ukanushaji kwa Kuzingatia Nyakati na Hali

## Ukanushaji

### I. Nyakati

### 1. Wakati uliopita

### Zoezi la 1

**1. Majibu yanayopendekezwa:**

*hakikuvunjika, hakuja, hatukufika, hapakuoshwa, hukuwaka, hayakuchomwa, hukupandwa, haikushonwa*

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Mimi sikumsaidia kubeba mawe hayo.

(b) Gari halikupeleka abiria Moyale.

(c) Majirani zetu hawakuishi kwa uhasama.

(d) Kikapu hicho hakikumwaga mtama.

(e) Mwirigi hakufaulu kupata kazi hiyo.

(f) Mvua haikunyesha usiku kucha.

(g) Kiti alichokalia hakikutengenezwa na Hamza.

(h) Mkutano wa amani hukufanywa jana uwanjani.

(i) Fulana hii haikununuliwa Mombasa.

(j) Sikutembelea Ziwa Naivasha.

**3.** (b) ***Majibu yanayopendekezwa:***

*Haikuwa, hakuja, hakuwa, hawakuwepo, hakuwa, hakuwa*

4. (a) *Tumia vintenzi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi*.

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 4 (a).*

## 2. Wakati uliopo

### Zoezi la 2

**1. Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| Hatuongei, halali, hazijengwi, haipandwi, hakipakuliwi, siji, havitatandikwa |

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Ligale hamfunzi Wandera kuendesha pikipiki.

(b) Michezo ya riadha haifanyiki nchini Ufaransa.

(c) Ulimi wake hauumi kwa sababu ya vidonda.

(d) Mbwa hachezi na paka.

(e) Ndoo ya maziwa haivuji.

(f) Kucheka kwake hakupendezi.

(g) Chuo hiki hakifunzi masomo mengi.

(h) Kato hamtembelei shangazi yake.

(i) Hatutenganishwi na mizozo yoyote.

(j) Asali ya babu hairambwi na Akoko.

**3.** (b) ***Majibu yanayopendekezwa:***

*Haendeshi, Hana, hawampi, hawana, hawangojei, haelewi, hawaogopi, hafi*

4. (a) *Tumia vitenzi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi*.

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 4 (a)*.

## 3. Wakati ujao

### Zoezi la 3

**1. Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| Hatutapanga, hawataomba, hutatibiwa, haitaharibika haitaandikwa, hakutafurahisha, hapatafaa |

**2. Majibu yanayopendekezwa**:

(a) Mama hataninunulia baiskeli.

(b) Chakula hakitapikwa na Kiende.

(c) Ukweli huu hautamfurahisha mwalimu.

(d) Gazeti la baba halitaletwa na Kaiyongi.

(e) Nyumba yetu haitapakwa rangi nyeusi.

(f) Mwanafunzi yule hataanguka mtihani.

(g) Shamba letu halitapandwa mahindi.

(h) Mpira wa Kaumbuthu hautachezwa na watoto.

(i) Majirani hawataandaa mkutano.

(j) Sitampelekea nguo zake kwa fundi.

**3. (b) Majibu yanayopendekezwa:**

*Hakutakuwa, hawataruhusiwa, hazitakubaliwa, hayataegeshwa, hawatakuwa, haitafungwa*

4. (a) *Tumia vitenzi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi*.

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 4 (a*).

## II. Hali

### 1. Hali ya mazoea

### Zoezi la 4

**1. Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| hapandi, hanyoi, hatazami, hategi, hanunui, hachinji |

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Nyinyi hamruhusiwi kupiga picha hapa.

(b) Maua haya hayasafirishwi hadi Ulaya.

(c) Keki ya harusi haipikwi na Kigara.

(d) Jina lake haliandikwi hivi.

(e) Yeye haongei kwa haraka.

(f) Tamaduni zilizopitwa na wakati haziruhusiwi na serikali.

(g) "Yeye hafungui duka lake mapema," jirani aliniambia.

(h) Simu hii haipigwi mara kwa mara.

(i) Kemunto hafanyi biashara mjini Kisii.

(j) Chai tunayokunywa asubuhi haipikwi kwa maziwa.

3. (a) *Tumia vitenzi ulivyopewa kutunga sentensi sahihi.*

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 3 (a*).

## 2. Hali timilifu

## Zoezi la 5

### 1. Majibu yanayopendekezwa:

| |
|---|
| haujakatwa, hakijakanyagwa, hatujacheza, hazijavutwa, hamjafeli, hajajiunga |

### 3. Majibu yanayopendekezwa:

(a) Kwaya haijaimba wimbo wa sifa.

(b) Sijajua Kilonzo hajaiba pesa hizo.

(c) Karolina hajashinda mchezo huo.

(d) Nguo zilizoanikwa hazijakauka.

(e) "Kwa nini mama hajaalikwa katika harusi hiyo?" Kanario aliuliza.

(f) Jina la mwenye gari halijaandikwa kwenye mlango wa gari.

(g) Ni wanafunzi wangapi hawajafika?

(h) Salaale! Shule yetu haijashinda mchuano huo.

(i) Viatu vya Linet havijararuriwa na mtoto.

(j) Mizinga iliyo shambani haijajaa asali

## 3. Hali ya masharti ya -nge-

### Zoezi la 6

#### 1. Majibu yanayopendekezwa:

1. asingenunua, usingekatwa, usingepikwa, isingetosha, yasingekatwa, msingeingia,
2. zisingeanikwa, wasingekosea, lisingefunikwa

#### 2. Majibu yanayopendekezwa:

(a) Mwalimu alimwambia Ntinyari, "Usingejikakamua usingeshinda."

(b) Asingeongea kwa sauti asingesikika.

(c) Chumba kisingepangwa vizuri kisingetoshea wageni.

(d) Usingekunywa chai moto usingechomeka ulimi.

(e) Harusi ya Mepukori na Wacera isingefanyika tusingefurahia.

(f) Wasingeuimba wimbo huo wasingetambuliwa.

(g) Shangazi asingetutembelea asingetuletea pipi.

(h) Mguu wake usingepona asingecheza futiboli.

(i) Sote tusingechukiana dunia isingekuwa na vita.

(j) Wananchi wasingeandamana biashara nyingi zisingefungwa.

#### 3. Majibu yanayopendekezwa:

(a) Msingekimbia msingefika mapema.

(b) Wasingelima shamba hilo wasingevuna mazao mengi.

(c) Nisingekuwa na nidhamu nisingezawadiwa.

(d) Kathuure asingemaliza kuosha asingepumzika.

(e) Tusingekuwa na runinga tusingetazama kipindi hicho.

(f) Jua lisingewaka tusingeanika mpunga.

(g) Usingekuwa na mbio usingeshiriki mashindano ya riadha.

(h) Mburugu asingeruka juu zaidi asingefikia paa la nyumba.

(i) Tusingelala mapema tusingeamka alfajiri.

4. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoonyesha -nge- ya masharti kutunga sentensi sahihi.*

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 4 (a).*

5. *Andika kifungu kifupi ukitumia ukanushaji wa -nge- ya masharti.*

## 4. Hali ya masharti ya -ngali-

### Zoezi la 7

1. **Majibu yanayopendekezwa:**

| |
|---|
| wasingalipika, isingalikatwa, lisingaliwaka, yasingalinukia, visingalizuka, isingalifunguliwa, kusingalikalika, usingalikatika |

2. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Tawi hili lisingalikatwa lisingaliangukia paa.
(b) Kutembea kwake kusingalikuwa kwa haraka asingalimfikia.
(c) Uchoyo wa watu hao usingalipungua wasingalipendwa.
(d) Waraka huu usingalifika mapema nisingalichangiwa hela za kujiunga na chuo kikuu.
(e) Maharagwe yasingalipikwa vizuri yasingalilika.
(f) Tusingalimwona tusingalimsalimia.
(g) Yeye asingalirejea nchini asingaliteuliwa kuwa waziri.
(h) Msitu usingalichomeka wanyama pori wasingaliangamia.
(i) Mkewe Luka asingalisoma asingalikuwa meneja wa benki.
(j) Pikipiki yake isingaliibiwa asingaliteseka sana.

3. **Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Sharleen asingalijua umuhimu wa elimu asingalisoma kwa bidi.
(b) Mtoto mkorofi asingalipigwa ikiwa asingaliiba simu.
(c) Serikali isingalijenga shule nyingi watoto wengi wasingalisoma.
(d) Dereva asingalivunja sheria za barabarani asingalikamatwa.
(e) Magunia haya yasingaliwekwa nafaka yasingalishonwa.

(f) Mashabiki wasingalifika uwanjani wachezaji wasingalifurahi.

(g) Msingalinisubiri nisingaliwabeba kwa gari langu.

(h) Asingaliongea naye kwa heshima asingalikubaliwa kuingia.

(i) Karamana asingalikuwa na watoto wachache asingaliwalea vyema.

(j) Stesheni ya redio isingalicheza muziki wa kupendeza nisingaliisikiliza.

4. (a) *Tumia vitenzi vyovyote vinavyoonyesha -ngali- ya masharti kutunga sentensi sahihi*.

(b) *Kanusha sentensi ulizotunga katika nambari ya 4 (a).*

5. *Andika kifungu kifupi ukitumia ukanushaji wa -ngali- ya masharti*.

## 5. Hali ya masharti ya -ki-

### Zoezi la 8

#### 1. Majibu yanayopendekezwa:

| |
|---|
| zisipojengwa, kusipolimwa, msipomwambia, yasipochotwa, wasipofurahia, tusiposema, usipochaguliwa, kisipoliwa |

#### 2. Majibu yanayopendekezwa:

(a) Maji <u>yasipokupwa</u> baharini **ha**tutaogelea.

(b) Kaari <u>asipofika</u> Jumamosi **ha**talipwa hela zake.

(c) <u>Usipoongea</u> vizuri **hu**taeleweka.

(d) Mazingira <u>yasiposafishwa</u> wadudu **ha**wataisha.

(e) Mchele <u>usipopikwa</u> kwa nazi **hu**takuwa mtamu sana.

(f) <u>Usipomkanyaga</u> nyoka **ha**takuuma.

(g) <u>Tusipowapenda</u> wenzetu Mola **ha**tatubariki.

(h) <u>Usipotembea</u> bila umakinifu **hu**tapotea jijini.

(i) <u>Usipopiga</u> kelele mahakamani **hu**takamatwa.

(j) <u>Usipolipa</u> deni **hu**takopeshwa tena.

**3. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Usipowazia swali hilo hutapata jawabu.

(b) Wanawake wasipoheshimiwa familia hazitakuwa na amani.

(c) Jogoo asipowika mimi siamki.

(d) Rais asipofungua hafla hii michezo haitaanza.

(e) Simba asipounguruma mimi sitetemeki.

(f) Matatu isipoondoka mapema haitaniacha.

(g) Kagwiria asiponitembelea hataniletea vibanzi.

(h) Mwanariadha asipovunja rekodi ya dunia hatapewa mamilioni ya pesa.

(i) Nisipoandika kitabu hiki hakitasomwa kote nchini.

(j) Mtoto asipolia mamake hatamnyonyesha.

4. (a) Tunga sentensi sahihi zinazoonyesha matumizi ya -ki- ya masharti.

(b) Kanusha sentensi ulizotunga katika namabri ya 4 (a).

5. Tunga kifungu kifupi ukitumia ukanushaji wa -ki- ya masharti.

## Zoezi la Marudio 12

**Majibu yanayopendekezwa:**

1. (b)

| | **Ukanushaji wa wakati uliopita** | **Ukanushaji wa wakati uliopo** | **Ukanushaji wa wakati ujao** |
|---|---|---|---|
| (i) | hatukuwa | hatuna | hatutakuwa |
| (ii) | haikuwa | hawana | sitakuwa |

**2. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Nyinyi hamkutakiwa msome hadithi mbili.

(b) Mkutano huo hutapangwa na chifu.

(c) Nyoka aliyeonekana hapa hakuingia kichakani.

(d) Pesa hizi hazifai kutumiwa kununua chakula.

(e) Harusi ya Kananu haitafanyika Jumamosi.

(f) Belinda haandiki barua kwa kutumia tarakilishi.

(g) Watu wengi hawatatazama mechi hiyo ya fainali.

(h) Mabati ya kujenga choo hicho hayakununuliwa jana.

(i) Ole Kina hachungi ng'ombe wake.

3. (b)

| | **Ukanushaji wa hali ya mazoea** | **Ukanushaji wa hali timilifu** |
|---|---|---|
| (i) | Halifanyii | Halijakuwa |
| (ii) | Hapendi | Hajaenda |
| (iii) | Hatoi | Hajaamini |

**4. Majibu yanayopendekezwa:**

(a) Sijarudi kutoka Uingereza.

(b) Tarumbeta hailii wacheza ngoma wanapoingia jukwaani.

(c) Mwanafunzi gani hajalipiwa karo na mhisani?

(d) Ogachi hajapanda juu ya mwembe wenye maembe mabivu.

(e) Migogoro ya kijiji hiki haitatuliwi na wazee mara tu inapotokea.

(f) Matwana hii haipiti hapa kila asubuhi na jioni.

(g) Ziara yetu haijaahirishwa hadi mwezi ujao.

(h) Gavana hajafungua jengo jipya la kufanyia biashara.

(i) Wajukuu hawa hawasikilizi hadithi za babu kila jioni.

5. (b)

| Ukanushaji | | | |
|---|---|---|---|
| | **Hali ya masharti ya -nge-** | **Hali ya masharti ya -ngali-** | **Hali ya masharti ya -ki-** |
| | nisingekuwa | asingalikuwa | asipomnunulia<br>**ha**takuwa<br>usipokuwa<br>**hu**tabarikiwa |

6.

(a) Meno yake yasipong'oka hataweza kula nyama.

(b) Rais wetu asingetutembelea asingeelewa kiini cha matatizo yetu.

(c) Asingaliachana na pombe mapema asingaliokoa maisha yake.

(d) Mbu wasingeisha tusingelala usingizi mnono.

(e) Uchaguzi usipokaribia kampeni hazitaanza.

(f) Tusingalikuwa na nguvu za umeme tusingalikuwa na maisha mazuri.

(g) Wafisadi wote wasiposhtakiwa uchumi wetu hautaimarika.

(h) Muthuku na Kiome wasingalikubaliana kuhusu mpaka wao ugomvi wao usingaliisha.

(i) Nisingekuwa na uwezo nisingemsaidia yule mtoto anayerandaranda mjini.

## 8. Aina za Sentensi

### I. Sentensi sahili

### Zoezi la 1

1. (a) Miti imepandwa.

(b) Watoto wanafahamishwa kuhusu haki zao.

(c) Tunapaswa kuwatunza wanyama.

(d) Linda amenawa mikono kwa sabuni na maji.

(e) Watoto watawasaidia wazazi wakati wa likizo.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Ninatembea.

(b) Muuguzi alikuwa akimnywesha mtoto mgonjwa dawa.

(c) Mhalifu ametiwa mbaroni.

(d) Msitu huo una machimbo yenye madini mengi.

(e) Waziri na mhandisi wanakagua kiwanda kipya.

### II. Sentensi ambatano

### Zoezi la 2

1. (a) Ugonjwa huo ni hatari lakini si rahisi kuusambaza.

(b) Fagia sakafu kisha uzoe taka zote.

(c) Misitu ni maliasili, maziwa na mito ni maliasili pia.

(d) Unambebesha punda mzigo mzito ilhali amechoka.

(e) Zungumza naye taratibu kwa vile ana huzuni leo.

**2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:**

(a) Mvua imepusa kwa hivyo wakulima wameanza kupanda miti.

(b) Lonare anakuna nazi na Kamene anadondoa mchele.

(c) Wanafunzi walifika shuleni ila hawakufunzwa.

(d) Wananchi walimchagua kisha akahamia mjini mara moja.

(e) Baraka alikuwa mhitaji lakini hakujaribu kuiba hata siku moja.

3. (a) Riziki analia kwa hivyo Rehema anamliwaza.

(b) Ndege imetua na abiria wameshuka./Kwa kuwa ndege imetua, abiria wameshuka.

(c) Watoto wanasoma vitabu vya hadithi huku wengine wakicheza mpira uwanjani./Watoto wanasoma vitabu vya hadithi bali wengine wanacheza mpira uwanjani.

(d) Pundamilia ni mnyama wa mwituni ila punda hufugwa.

(e) Chungwa ni tamu bali/ ilhali/lakini limau ni chachu.

(f) Mtoto ana afya nzuri kwa vile/kwa kuwa/kwa sababu amekuwa akilishwa vizuri.

## III. Sentensi changamano

### Zoezi la 3

1. (a) Ugonjwa ambao umezuka mpakani utakabiliwa na wahudumu wa afya.

(b) Wangearifiwa mapema wangewekeza rasilmali ya kutosha.

(c) Watoto walibeba matunda walipoenda shuleni.

(d) Watu walioweka akiba katika benki wamelipwa fidia.

(e) Tuliona wanyama wengi tulipozuru mbuga ya Tsavo.

### 2. Majibu yanayotarajiwa ni kama vile:

(a) Magari yaliyoegeshwa chini ya mti yaliondolewa na askari.

(b) Mvua kubwa ambayo ilinyesha ilijaza mabwawa yote.

(c) Askari wangewajibika usalama ungeimarishwa.

(d) Vijana hao wangesikilizwa maandamano hayangetokea.

(e) Mwanafunzi aliyeandika insha nzuri ametuzwa na mwalimu.

## IV. Sentensi tata

### Zoezi la 4

1. (a) Wameahidi kutupeleka kwao.

(b) Chokea amenitupia tiara.

(c) Niliona kaa kando ya bahari.

(d) Wageni wa Maria na Juma wamefika.

(e) Mtoto amemkimbilia nyanya.

### Zoezi la Marudio 13

1. (a) Sentensi sahili ni sentensi yenye wazo moja.

(b) Sentensi ambatano ni sentensi yenye sentensi sahili mbili au zaidi na sentensi hizi huunganishwa kwa kiunganishi ama koma.

(c) Sentensi changamano ni sentensi ambayo imeundwa kwa sehemu mbili ambazo moja hutoa wazo lililo kamili ilhali nyingine haitoi wazo lililokamilika.

(d) Sentensi tata ni sentensi iliyo na maana zaidi ya moja.

2. (a) sahili

(i) Mhandisi anakarabati mtambo kiwandani.

(ii) Mfereji umevunjika.

(iii) Sudi anamsafisha mbwa wake.

(b) ambatano

(i) Kipindi kimekamilika na mwalimu ameondoka.

(ii) Wavulana wanafyeka nyasi na wasichana wanalengeta ua.

(iii) Mkurugenzi amepokea simu na kutoka ofisini.

(c) changamano

(i) Dawa zilizoagizwa na daktari zimeletwa leo.

(ii) Watalii waliotarajiwa wamefika hotelini.

(iii) Mawaziri ambao walichaguliwa wameanza kazi.

(d) sentensi tata

(i) Binti alimsomea Kibwana.

(ii) Mlango ulipofunguliwa aliingia mama aliyembeba mtoto na bwanake.

(iii) Mutuma alirudi kwao.

3. (a) Wananchi wote wamelipa ushuru.

(b) Kiranja amepeleka vitabu ofisini.

(c) Ukambi umethibitiwa nchini.

(d) Soipan anafanya mazoezi ya viungo vya mwili.

(e) Ndovu alikuwa akinywa maji.

(f) Nyumba yetu imepakwa rangi.

4. (a) Lila alimnyanyasa Dete hatimaye akachukuliwa hatua za kisheria.

(b) Leshau anamkama ng'ombe na Loitemu anawalisha ndama.

(c) Kiboko huishi majini, sungura huishi mwituni.

(d) Habona na Hirbo wanazozana ingawa chifu alikuwa amewapatanisha.

(e) Salma amefua nguo zote kisha akazianika juani.

5. (a) Mashine tulizonunua zilitumika kiwandani.

(b) Nyumba zilizojengwa na kiongozi zimeuzwa.

(c) Tukio ambalo lilisababisha mzozo lilitatuliwa.

(d) Bahari ikiwa shwari tutaogelea.

(e) Kama watashauriwa, watakuwa waadilifu maishani.

(f) Licha ya kuonywa mara nyingi, alichelewa kufika kazini.

6. (a) Njeri amembebea Lona vitabu.

(b) Muna amemrithisha Wafula nyumba yake.

(c) Umeona mamba?

(d) Tazama kipusa.

(e) Amepata kima leo.

7. (a) Sentensi sahili

(i) Kumekucha.

(ii) Sifa ameamka.

(iii) Jua linachomoza taratibu katika mtaa wa Mtongole.

(iv) Anafanya mazoezi kwa muda wa nusu saa.

(v) Katika mijadala yao walikosoana kwa amani na upendo.

(b) Sentensi ambatano

(i) Sifa anaketi kitandani na kunyosha mikono yake juu ya kichwa chake.

(ii) Anafahamu kuwa ili awe na afya bora na mapumziko ya kutosha, sharti alale mapema.

(iii) Pia walielekezwa kufanya mazoezi ya viungo vya mwili ili kuvinyosha na kupunguza uto mwilini.

(iv) Alisogea dirishani na kuangalia ua karibu na dirisha.

(v) Aliingia bafuni akaoga kisha akaingia jikoni na kujitayarishia kopo la uji.

(vi) Hatimaye alikaa mezani na kutwaa tarakilishi.

(vii) Walipaswa kutambua aina mbalimbali za sentensi kutoka kwenye kifungu hicho kisha wapige chapa na kuwatumia wanakikundi mtandaoni ili wazitolee sentensi hizo maoni.

(viii) Walishauriwa kupata lishe bora na kuzingatia usafi wa mwili na mazingira ili wajiepushe na magonjwa ya kuambukizwa kama vile mafua, kipindupindu na hata kifua kikuu.

(c) Sentensi changamano

(i) Usiku uliotangulia alikuwa amelala mapema kama ilivyokuwa kawaida yake.

(ii) Anayekosa kuzingatia afya bora huathirika pakubwa.

(iii) Siku iliyotangulia walikuwa wamefunzwa kuhusu magonjwa yanayoambukizwa na kukumbushwa kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa na magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha.

(iv) Alishiriki sana kwenye mijadala waliyokuwa nayo kwenye vikundi darasani mwao.

(v) Alifurahia sana mawazo ya wenzake jinsi nao pia walivyofurahia mawazo yake.

(vi) Alipokuwa akijongea dirishani aliona chombo alichokuwa hajakirudisha kilipofaa kuwepo.

(vii) Alitaka kukamilisha kazi waliyopewa na mwalimu.

(viii) Walipewa kifungu kilichokuwa kinazungumzia masuala ya afya.

(ix) Baada ya likizo yao fupi mwalimu angehakiki majibu yao.

(d) Sentensi tata

(i) Alisogea dirishani na kuangalia ua karibu na dirisha.

(ii) Mjomba alimpa tarakilishi yake.

(iii) Alipokuwa akijongea dirishani aliona chombo alichokuwa hajakirudisha kilipofaa kuwepo.

## 9. Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa

### A. Usemi halisi

### Zoezi la 1

1. Usemi halisi ni nukuu ya maneno halisi yaliyosemwa na msemaji bila kuongeza au kutoa chochote.
2. Rejelea Kitabu cha Mwanafunzi uk. wa 142 – 143.
3. Sentensi za usemi halisi ni: (a), (b), (d), (f), (i), (j).

### Zoezi la 2

1. (a) "Hakika Mungu si Athumani," kijana alijisemea.

   (b) "Nitashiriki mbio za nyika zijazo," mwanariadha aliahidi.

   (c) Wageni walisema, "Tutawatembelea kesho jioni."

   (d) Tume ya Uchaguzi ilitangaza, "Uchaguzi utafanyika mwaka ujao."

   (e) "Nitawajibikia majukumu yangu," Jaji Mkuu alitoa hakikisho.

2. (a) "Simameni!" kocha aliwaamuru wachezaji wake.

(b) "Tulifika bila kuchelewa," alisema Naipanoi.

(c) "Kila mwanafunzi anafaa kusajiliwa upya," Waziri wa Elimu aliagiza.

(d) "Enda dukani ununue mkate, majani na siagi," baba alisema.

(e) Bawabu alimjibu, "Aliingia punde tu ulipotoka."

(f) "Ukifika nyumbani vua sare ya shule," mama alinikumbusha.

(g) "Je, unafahamu jiji kuu la Kenya?" Toni alimwuliza Kendi.

(h) Waimbaji waliimba, "Maadili ya kitaifa ni nguzo muhimu."

(i) Mteja aliuliza mpishi, "Unapika nini?"

(j) "Nyote mnakaribishwa, "Shangazi alitwambia."

3. *Tunga sentensi kumi sahihi katika usemi halisi*.

## B. Usemi wa taarifa

### Zoezi la 1

1. Usemi wa taarifa ni ripoti au maelezo ya maneno yaliyosemwa na mtu mwingine.
2. Rejelea Kitabu cha Mwanafunzi uk. wa 145 – 147.
3. Sentensi za usemi wa taarifa ni: (b), (d), (e), (g), (h), (j).

### Zoezi la 2

1. *Andika sentensi kumi sahihi kisarufi na kimantiki katika usemi wa taarifa*.
2. (a) Mshambulizi alisema Alhamdulilahi baada ya kufunga bao.

   (b) Aliwafahamisha kuwa wao walikuwa ndugu wa toka nitoke.

   (c) Alimwambia nduguye kuwa alifika mjini salama salmini.

   (d) Alisikika akisema kuwa siku hiyo ilikuwa siku hiyo na aliyekuwa akisema siku iliyofuata alikuwa mwongo.

   (e) Imamu aliwasihi kwa kuwaambia wakumbuke kuwafaa waliokuwa na mahitaji katika jamii.

   (f) Alijibu kuwa yule alikuwa mwanafunzi wa mwaka wa pili.

   (g) Andere alikiri kuwa alikuwa ameishi humo tangu mwaka uliotangulia.

   (h) Daktari alishangaa kuwa alidhani maradhi yale hayakuwa ya kuambukizwa.

   (i) Mgeni aliwaambia kuwa kwao ilikuwa ni nchi jirani.

   (j) Mke alimuaga mumewe kwa kumtakia safari njema.

### Zoezi la Marudio 14

1. Usemi halisi ni maneno halisi jinsi yalivyosemwa na msemaji ilhali usemi wa taarifa ni ripoti au maelezo kuhusu alichokisema msemaji. (Kubali majibu mengine ambayo ni maelezo ya tofauti kati ya usemi halisi na usemi wa taarifa.
2. *Tunga sentensi tano sahihi katika usemi halisi.*
3. *Badilisha sentensi ulizotunga katika nambari ya 2 ziwe katika usemi wa taarifa*.
4. (a) Mwalimu aliwaambia wanafunzi, “Fikeni mapema kesho.”

   (b) “Msikose maadili maishani,” walionywa.

   (c) “Niwie radhi kwa kosa ambalo nimefanya,” niliomba.

(d) “Ingieni kwenye lori!” askari aliwaamuru maabusu.

(e) Mhudumu alisema, “Mkifika nitawahudumia barabara.

(f) “Taarifa ya habari ya leo jioni itacheleweshwa,” mwanahabari alisema.

(g) “Ni muhimu kupanda miti,” mwanamazingira aliwakumbusha.

(h) “Nipikie uji wa muhogo,” mtoto alimwomba mama yake.

(i) Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi alitangaza, “Uchaguzi utarudiwa.”

(j) “Kwa nini mmechelewa leo?” chifu aliwauliza wanakijiji.

5. (a) Alimwuliza iwapo alimfahamu Mwalimu wake wa Kiswahili.

(b) Ayubu alimwambia Kiio kuwa kwao kulikuwa na milima na mabonde.

(c) Mshauri alisema kuwa baada ya dhiki ilikuwa faraja.

(d) Mwenyekiti alitangaza kuwa mkutano ambao ungefanyika siku iliyofuata ulikuwa umeahirishwa.

(e) Mkimbiaji aliulizwa iwapo alidhani angeshinda mbio hizo.

(f) Aliagiza waondoke hapo upesi.

(g) Bawabu alimwuliza kijana alikokuwa anatoka na alikoelekea.

(h) Baba alitamka kwa kushangaa kwamba alikuwa akiamka wakati jua lilikuwa limewaka tayari.

(i) Waliitikia kwa kusema ndio walikuwa tayari.

(j) Mwuguzi alimwambia akumbuke kumeza dawa hizo kuanzia siku iliyofuata kulingana na maagizo ya daktari.